# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

SHULE YA SEKONDARI ZEBEYA,

S.L.P 184,

**MASWA – SIMIYU.**

SIMU; 0627830521

Email. *1969lwangato3@gmail.com*

14/12/2020

***Kumb.Na.ZBYSS/ADM/48/VOL1........................***

**JINA LA MWANAFUNZI**

..........................................................................................................

**S.L.P 170, MASWA.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ZEBEYA WILAYA YA MASWA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na **kidato cha kwanza (I)** katika shule hii mwaka **2021** Shule ya Sekondari **Zebeya** ipo katika **kata ya Senani.**

Muhula wa kuanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **24/01/2021**.

Mambo muhimu ya kuzingatia

**SARE YA SHULE**

**(A) WASICHANA**

i. Sketi mbili nyeusi kitambaa cha suti siyo sukari –sketi ziwe za rinda boksi ndefu iguse kisigino cha mguu, kitambaa kimeambatanishwa kwenye fomu.
ii. Shati mbili (2) Tetroni za mikono mifupi; zisishonwe za kubana mwili na ziwe ndefu za kuchomekea wakati wote.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu visivyo na urembo wala visigino virefu vyenye kamba.
iv. Soksi ndefu jozi mbili rangi nyeupe.
v. Sweta mbili rangi ya bluu.

NB.Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule.

### (B) WAVULANA

i. Suruali mbili nyeusi zenye marinda yasiyozidi mawili na mifuko mitatu isiyo ya kubandika isiwe ya kubana iwe yenye kitambaa cha Suti.
ii. Shati mbili nyeupe tetroni zenye mikono mifupi.
iii. Viatu vyeusi vya Ngozi -vyenye kamba ,visivyo na sori ndefu au nene
iv. Soksi ndefu jozi mbili nyeusi.
v. Mkanda wa ngozi usiwe na chuma kikubwa.
vi. Sweta mbili rangi ya bluu.

TANBII: Suruali za jeans haziruhusiwi.

### (C) MAVAZI YA KAZI NA MICHEZO.

**WASICHANA.**

Sketi nyeusi,raba nyeusi na tisheti ya rangi nyekundu yenye kora

**WAVULANA.**

Suruali nyeusi,raba nyeusi na tisheti ya rangi nyekundu yenye kora

**KWA WOTE**: Suruali au track rangi nyekundu )

**MAHITAJI MENGINE**;

Waje na ndoo ndogo na mfagio wa chelewa

**MAHITAJI YA TAALUMA**

- **Mfuko wa kubebea daftari(school bag)**
- **Bofa(mathematical set)**
- **Dictionary(kamusi)**
- **Daftari ishirini(20)**

## 3.1 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978**.Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi nchini.sharia na kanuni muhimu za shule ni:-

a) Heshima kwa viongozi,wazazi wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule,na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo.
e) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
h) Kutunza mali za umma

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bagi, cocaine, mirungi, kubeli na kadharika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kutoa mimba.
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
l) Kuwa na simu ya mkononi

**Naambatanisha na fomu zifuatazo**;

Medical Examination Form ambayo itatakiwa kujazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Pia fomu hii aje nayo mwanafunzi siku ya kuripoti shuleni.

Naambatanisha pia fomu ya historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezoYanayotolewa shuleni

Siku ya kuripoti mwanafunzi aje shuleni na mzazi au mlezi

Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

...........................

***JOSEPH MTAKI LWANGATO***
***MKUU WA SHULE***

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ZEBEYA
MASWA

**FORM B**

**MASWA DISTRICT COUNCIL**

SALAGE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 274,
**MASWA – SIMIYU.**

DATE: ................................

TO THE MEDICAL OFFICER,
...........................................
...........................................
...........................................

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine the below mentioned girl/boy as to her/his fitness for studies in this school.

(This form must be completed by a government medical officer)

Student's full name: ____________________

Present age: ____________________

Blood Test: ____________________

Stool Examination: ____________________

T.S. Test: ____________________

Asthma: ____________________

Eye Disorder: ____________________

Skin Diseases: ____________________

Anemia: ____________________

Chest: ____________________

Pregnancy test for girls: ____________________

Operations: ____________________

Serious accidents: ____________________

Physical defects or impairment: ____________________

Any other infections/Deseases: ____________________

I certify that I have personally examined Mr/Miss ____________________ and found his/he fit to pursue further studies.

Signature ____________________ Designation ____________________

Official stamp: ____________________

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUFUATA SHERIA ZA SHULE.**

1. Jina la Mwanafunzi ..........................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa: ...........................
3. Shule ya Msingi:................................. Namba ya Mtihani ........................
   Kata ya ........................................... Tarafa ....................................
4. Jina kamili la baba: ........................................................... Hai / amefariki
   Kijiji ................................ Kata ......................... Tarafa ........................
5. Jina kamili la Mama: .......................................................... Hai / amefariki
   Kijiji .................................. kata ...................... Tarafa ........................
6. Jina kamili la mlezi (kama hana mzazi) ..............................................
7. Uhusiano na mlezi ...........................................................................
8. Kazi ya Baba / Mlezi ........................................................................
9. Jamaa katika familia:-
   (a) Jina la ndugu wa karibu .....................................
   (b) Jina la ndugu wa karibu .....................................
   (c) Yeye ni wa ngapi katika familia ...................................

***NB***: Nathibitisha kuwa nimesoma na kuelewa vizuri sheria za shule hii na kwamba nathibitisha kuwa sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Ee Mungu nisaidie.

...................................
Sahihi ya Mwanafunzi.